
Haliuzwi
MACHI 4, 2026
/islamicftz
Ramadhan 15 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 572
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Mwenyekiti wa Bodi ya Wazazi Shule ya Imaan apigia debe shule za Kiislamu

# Mwinyi ahimiza ufadhili miradi vyuo vya Qur'an



## The Islamic Foundation yafuturisha familia 600 Kigoma

يا أيها الذين آمنوا كتب عليكم الصيام كما كتب على الذين من قبلكم

Nasaha za wiki »

Malezi / familiya »

## Nchi za Ghuba zaimarisha mshikamano kukabiliana na Iran

MZOZO MASHARIKI YA KATI:

## Rais samia aagiza kuimarisha akiba ya kimkakati ya mafuta






"Kama tunavyoona misukosuko iliyotokea hapa karibuni wiki iliyopita na tunayoendelea nayo, tayari imeshapandisha bei ya mafuta kwa 13% hadi jana, sasa hatujui leo na siku zijazo lakini tumuombe Mungu watu wale wakae juu ya meza wazungumze wakubaliane"

Rais Samia Suluhu Hassan

## Vizuizi vikali Ramadhan ndani ya Masjid Al Aqswa

SAMRATH MSUYA



# Mwinyi ahimiza ufadhili miradi vyuo vya Qur'an

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, amewataka wadhamini na Waislamu wenye uwezo kuunga mkono miradi ya elimu ya Qur'an nchini ili kuimarisha malezi ya dini kwa maslahi ya kizazi kijacho.

Dkt. Mwinyi alitoa kauli hiyo wakati wa Mashindano ya Kimataifa ya Qur'an kwa njia ya Tajweed kwa mwaka 2026M sawa na 1447H yaliyoandaliwa na Taasisi ya Khidmatul Qur'an Islamic Foundation na kufanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC).

Alisema miradi inayotekelezwa na taasisi hiyo ikiwemo ujenzi wa skuli ya Qur'an, ujenzi wa msikiti huko Kigamboni na kituo cha masomo ya dini inahitaji kuungwa mkono zaidi ili kuendeleza mafanikio ya mashindano hayo.

"Niwaombe wadhamini wawe mstari wa mbele kudhamini miradi inayotekelezwa nje ya mashindano haya... hatuwezi kufika hapa bila kuwa na skuli za Qur'an na vituo vya kusomesha vijana wetu," alisema Rais huyo anayejulikana kwa mapenzi yake makubwa na Qur'an.

## Aenzi wageni wa Qur'an

Katika hatua nyingine, Rais Dkt Mwinyi aliwashukuru washiriki na majaji kutoka nje ya Tanzania akisema ujio wao umeongeza hadhi ya mashindano hayo na kuyafanya yawe ya kimataifa zaidi. "Kipekee napenda kuwashukuru wageni wetu kutoka nje ya Tanzania kwa kukubali kushiriki. Ushiriki wao unayapa hadhi mashindano haya na kuyafanya yakidhi vigezo vya kuitwa ya kimataifa," alisema.

Mashindano hayo yaliwakutanisha wasomaji wa Qur'an kutoka nchi mbalimbali ikiwemo Iraq, Misri, Indonesia, Malaysia, Morocco, India, Afghanistan, Pakistan, Afrika Kusini pamoja na Tanzania na Zanzibar.

Kila mshiriki alipewa dakika nane hadi kumi kusoma Qur'an kwa kuzingatia kanuni za tajweed mbele ya jopo la majaji wanne kutoka Misri, Libya na Tanzania.

Mwisho wa mashindano hayo, mshiriki kutoka Misri, Ashraf Seif Saleh maarufu Bilal Seif, aliibuka mshindi wa kwanza na kujinyakulia dola 5,000, akifuatiwa na Mohammad Hussein Mahmur kutoka Malaysia aliyeshika nafasi ya pili na zawadi ya dola 3,000.

Mshiriki mwenyeji wa Tanzania, Hussein Qays, alishika nafasi ya tatu kwa alama na kujishindia dola 2,000.

Taasisi ya Khidmatul Qur'an Islamic Foundation ilianzishwa takribani miaka 20 iliyopita na Ali Mohammed Saleh kwa lengo la kukuza elimu ya Qur'an na kuendeleza mashindano ya kimataifa ya usomaji wa Qur'an.

DAR ES SALAAM

NA YUSUPH AMIN

## MZOZO MASHARIKI YA KATI:

# Rais samia aagiza kuimarisha akiba ya kimkakati ya mafuta

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameiagiza Wizara ya Uchukuzi kuimarisha akiba ya kimkakati ya mafuta ili kuongeza uthabiti wa taifa dhidi ya misukosuko ya kimataifa inayoathiri bei ya nishati katika soko la dunia.

Akizungumza leo Machi 3, 2026 jijini Dar es Salaam wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi wa mradi wa ujenzi wa matanki ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika eneo la Kigamboni, Rais Samia amesema Tanzania haina budi kujiandaa mapema kukabili changamoto za mabadiliko ya bei yanayosababishwa na migogoro ya kimataifa.

Ameeleza kuwa misukosuko iliyojitokeza wiki iliyopita katika baadhi ya nchi tayari imechangia kupanda kwa bei ya mafuta kwa takribani asilimia 13, hali inayoweza kuathiri gharama za maisha na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi.

"Tumuombe Mungu watu wale wakae mezani wazungumze, wakubaliane, misukosuko hii iishe ili dunia irudi katika hali yake ya kawaida ya kuendesha chumi za nchi zetu," amesema Rais Samia.

Rais Samia amesisitiza kuwa uwekezaji katika miundombinu ya kisasa ya kuhifadhi mafuta ni hatua ya kimkakati ya kuimarisha usalama wa nishati nchini na kulinda uchumi dhidi ya athari za mabadiliko ya ghafla ya bei katika soko la kimataifa.

Aidha, ameongeza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya mkakati mpana wa Serikali wa kuhakikisha upatikanaji wa nishati unakuwa wa uhakika, nafuu na endelevu kwa maendeleo ya viwanda, biashara na ustawi wa wananchi.

Mradi huo wenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 374,000 ambazo ni sawa na Lita milioni 378, unatarajiwa kuongeza uwezo wa taifa kuhifadhi akiba ya kimkakati, kupunguza utegemezi wa ununuzi wa dharura na kusaidia kudhibiti mishtuko ya bei kwa walaji wa ndani.



HABARI
MASHARIKI YA KATI

NA UKHTI FATIMA SS

# Nchi za Ghuba zaimarisha mshikamano kukabiliana na Iran



Nchi za Ghuba zimeanza kuonyesha mshikamano mkubwa wa kisiasa na kiusalama kufuatia mashambulizi ya Iran katika maeneo kadhaa ya Mashariki ya Kati, huku viongozi wa kanda hiyo wakisisitiza kulinda uhuru wa mataifa yao na utulivu wa eneo hilo.

Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Qatar, Bahrain na Kuwait zimelaani vikali mashambulizi ya Iran yaliyolenga miji na miundombinu muhimu katika kanda hiyo baada ya operesheni ya kijeshi ya Marekani na Israel dhidi ya Iran kuanza mwishoni mwa wiki.

Baraza la Ushirikiano la Ghuba (GCC) limesema mashambulizi hayo ni ukiukaji mkubwa wa uhuru wa mataifa na yanaweka hatarini usalama wa eneo zima. Mataifa hayo pia yamesisitiza kuwa hayakuruhusu ardhi au anga zao kutumiwa kushambulia Iran, lakini bado yamejikuta yakilengwa na mashambulizi ya kulipiza kisasi.

Katika ishara ya mshikamano wa kikanda, Rais wa UAE Sheikh Mohamed bin Zayed Al Nahyan alipokea simu kutoka kwa Mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed bin Salman, ambapo viongozi hao walijadili hali ya usalama na kulaani mashambulizi yaliyolenga UAE pamoja na nchi nyingine jirani. Saudi Arabia iliahidi kutoa msaada wote unaohitajika kusaidia kukabiliana na tishio hilo.

Viongozi hao pia walionya kuwa mashambulizi dhidi ya nchi jirani ni ukiukaji wa sheria za kimataifa na yanaweza kusababisha hatari kubwa kwa usalama na uthabiti wa Mashariki ya Kati.

Katika maeneo kadhaa ya Ghuba, mamlaka zimeanza kuchukua hatua za dharura kulinda raia. Qatar imewataka wakazi kubaki majumbani isipokuwa kwa dharura, huku Kuwait ikitangaza masomo ya vyuo vikuu kufanyika kwa njia ya mtandao hadi hali itakapotengamaa.

Nchini UAE, mamlaka za utalii zimeelekeza hoteli kuongeza muda wa kukaa kwa wageni waliokwama kutokana na kusimamishwa kwa safari nyingi za ndege. Takwimu zinaonyesha zaidi ya safari 1,500 za ndege zimefutwa katika nchi za Mashariki ya Kati kufuatia hali ya usalama.

Mashambulizi ya Iran pia yameathiri miundombinu ya kiuchumi, ikiwemo bandari na vituo vya biashara katika eneo la Ghuba, jambo linalozua wasiwasi mkubwa kwa uchumi wa kimataifa.

Hata hivyo, licha ya hali hiyo, nchi za Ghuba zimeonyesha msimamo wa pamoja wa kulinda mipaka yao na kushirikiana na washirika wao wa kimataifa ili kuhakikisha usalama wa kanda unaendelea kudumishwa. Wachambuzi wanasema mshikamano unaoonekana sasa kati ya mataifa ya Ghuba unaonyesha jinsi mashambulizi ya Iran yalivyoyaunganisha mataifa hayo, ambayo kwa miaka ya karibuni yalikuwa yakijaribu kuboresha uhusiano wa kidiplomasia na Tehran.

Kwa sasa, viongozi wa Ghuba wanaendelea kusisitiza umuhimu wa suluhisho la kidiplomasia lakini pia wakionya kuwa hawatasita kuchukua hatua madhubuti kulinda uhuru na usalama wa nchi zao.

HABARI MOROGORO

NA HASSAN NINGA, MOROGORO


















# Mwenyekiti wa Bodi ya Wazazi Shule ya Imaan apigia debe shule za Kiislamu

Jamii imetakiwa kuhakikisha watoto wanapata elimu inayozingatia misingi ya dini ya Kiislamu ili kujenga kizazi chenye maadili, nidhamu na uwajibikaji.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wazazi wa Shule ya Msingi Imaan iliyopo Kilakala, Manispaa ya Morogoro, chini ya Taasisi ya The Islamic Foundation, Mhandisi Abeid Mlapakolo, wakati wa mashindano ya kuhifadhi Qur'an yaliyowakutanisha wanafunzi, wazazi, walimu na wageni mbalimbali shuleni hapo.

Akizungumza kama mgeni rasmi, Mlapakolo alisema malezi ya mtoto si jukumu la shule pekee bali ni la jamii nzima, akisisitiza kuwa wazazi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha watoto wanapata elimu itakayowajenga kiroho, kiakili na kimaadili.

"Tunapowaleta watoto wetu katika shule hii ya Imaan, wanajengeka kiimani na kuweka msingi imara wa maisha yao ya baadaye. Elimu ya Qur'an inawafundisha nidhamu, heshima, uaminifu na uwajibikaji — sifa ambazo taifa letu linazihitaji kwa kizazi kijacho," alisema.

Aliongeza kuwa mashindano ya kuhifadhi Qur'an ni njia muhimu ya kuwajenga wanafunzi kiimani na kuwasaidia kujitambua mapema. Kwa mujibu wake, mtoto anayekua katika misingi ya dini huwa na uwezo mkubwa wa kujiepusha na mmomonyoko wa maadili unaoikumba jamii kwa sasa.

رمضان




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580







Mashindano ya kuhifadhi Qur’an yaliyowakutanisha wanafunzi, wazazi, walimu na wageni mbalimbali

UKHTI FATUMA SS

# Bopar aambia wafanyabiashara: Hamtafilisika kwa kutoa sadaka

Wafanyabiashara wametakiwa kujitokeza kusaidia shughuli za kueneza na kufundisha Qur'an badala ya kuwaacha wanaojishughulisha na kazi hiyo wakihangaika kutafuta msaada.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Bopar, Sheikh Said Nassir Nassor, wakati akizungumza katika Mashindano ya Kimataifa ya Qur'an kwa njia ya Tajweed yaliyofanyika katika Ukumbi wa JNICC jijini Dar es Salaam.

Alisema kusaidia shughuli za Qur'an hakusababishi mtu kufilisika bali huleta baraka na kuongezeka kwa mali.

"Wafanyabiashara wako wapi? Kwa nini tunawaacha watu wa Qur'an? Asifikirie mtu kuwa akiwasaidia atafilisika. Wallahi hawezi kufilisika," alisema.

Sheikh Nassor aliwataka Waislamu wenye uwezo kuungana kusaidia juhudi za kufundisha Qur'an hasa katika mwezi wa Ramadhan. "Tunawaacha watu wanadhalilika wakizunguka kuomba msaada. Hata mtu hana msahafu. Tunashindwa kununua msahafu? Kesho tutajibu nini mbele ya Mungu?" alisema.

Mashindano hayo yaliandaliwa na Taasisi ya Khidmatul Qur'an Islamic Foundation na kushirikisha washiriki kutoka nchi zaidi ya kumi.

Wadhamini wa tukio hilo pia walipata nafasi ya kuzungumza, akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Dkt. Abdulmajid Nsekela, aliyesema udhamini wa benki hiyo kupitia dirisha la huduma za Kiislamu la Albarakah ni sehemu ya kuitikia wito wa kuenzi Qur'an katika mwezi wa Ramadhan.

"Kuwa mwezi ambao iliteremshwa Qur'an, Ramadhan ni mwezi wa uongofu na upambanuzi, hivyo tukio hili ni mwitikio wa wito wa Mola wetu wa kushiriki na kuiheshimu Qur'an," alisema.

Kwa upande wake, mwakilishi wa Bakhressa Group, Mohammad Salum, alisema kuwekeza katika Qur'an ni kuwekeza katika maadili na mustakabali wa jamii.

## The Islamic Foundation yafuturisha familia 600 Kigoma

**Baadhi ya Waumini wa dini ya Kiislamu katika eneo la Mwasenga mkoani Kigoma wameishukuru Taasisi ya The Islamic Foundation kwa kuwajali makundi yenye uhitaji kwa kuwapatia futari katika mwezi mtukufu wa Ramadhan.**

**Waumini hao walitoa shukrani hizo walipozungumza na Gazeti Imaan mara baada ya kupokea msaada huo, wakisema umeleta faraja kubwa hasa kwa familia zenye kipato cha chini ambazo hukumbana na changamoto ya kupata futari ya uhakika.**

**Walisema msaada huo umefika kwa wakati muafaka kwani Ramadhan ni mwezi wa ibada, mshikamano na kusaidiana, hivyo kuguswa na taasisi hiyo ni ishara ya upendo na kujali jamii.**

**Aidha, waliwataka wadau na taasisi nyingine kuiga mfano huo kwa kuwasaidia wahitaji si katika mwezi wa Ramadhan pekee bali pia katika nyakati nyingine za mwaka.**

**Kwa upande wake, Mkurugenzi wa The Islamic Foundation Mkoa wa Kigoma, Omari Menshi, alisema familia 600 zimenufaika na msaada huo ambao unalenga kuendeleza moyo wa kusaidiana na kuwafariji wenye uhitaji.**

**Aliongeza kuwa futari hiyo imetolewa kwa ushirikiano na Taasisi ya Al-Baraka na imejumuisha mchele, maharage, mafuta ya kupikia, sukari, unga na tende.**






# Sekta fedha za Kiislamu yaingia hatua mpya ya ukuaji duniani

Sekta ya fedha za Kiislamu duniani inaingia katika awamu mpya ya maendeleo yakichochewa na mabadiliko ya teknolojia, mahitaji ya uwekezaji na msukumo wa uchumi endelevu.

Mtaalamu mwenye zaidi ya miaka 30 ya uzoefu katika sekta ya benki za Kiislamu katika nchi za Ghuba (GCC) wa benki za Kiislamu Syed Moosa Kaleem Al Falahi ameiambia tovuti ya Khaleej Times kuwa tasnia hiyo imebadilika kwa kiasi kikubwa kutoka kuwa huduma ndogo inayojikita zaidi katika kufuata masharti ya Shariah hadi kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa fedha duniani.

Alisema, katika hatua za awali taasisi nyingi za fedha za Kiislamu zililenga zaidi kuunda bidhaa zinazokubalika kwa mujibu wa Shariah na kuimarisha misingi ya kifedha ya benki. Hata hivyo, sasa sekta inaelekea katika uendelevu wa uchumi, matumizi ya teknolojia za kifedha na usimamizi imara wa hatari.

"Nimeona sekta hii ikibadilika kutoka huduma maalumu yenye mkazo wa kufuata kanuni za Shariah hadi kuwa nguzo muhimu ya mfumo wa fedha wa kimataifa. Hatua inayofuata ya ukuaji itaongozwa na uendelevu, ushirikiano na teknolojia," alisema Al Falahi, akizungumza katika mahojiano hayo yaliyoripotiwa na Khaleej Times.

Al Falahi alisema kuimarika kwa mifumo ya udhibiti na viwango vya kimataifa vinavyoongozwa na taasisi kama AAOIFI na Islamic Financial Services Board kumeongeza uwazi, utawala bora na kuimarisha imani ya wawekezaji katika sekta hiyo.

Akizungumzia mwenendo wa soko, Al Falahi alisema mahitaji makubwa yanaonekana katika utoaji wa hati za kifedha za serikali, mitaji ya benki kupitia sukuk, pamoja na uwekezaji katika miundombinu na miradi ya nishati safi. Miradi hiyo, alisema, inaendana vizuri na misingi ya fedha za Kiislamu pamoja na ajenda ya kimataifa ya maendeleo endelevu.

Al Falahi pia alisisitiza kuwa ili taasisi za fedha za Kiislamu ziendelee kuwa na ushindani duniani, zinapaswa kuendeleza bidhaa bunifu zinazozingatia Shariah, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kutumia teknolojia kuongeza ufanisi wa huduma.

Aliongeza kuwa usimamizi mzuri wa taasisi, uwazi katika mawasiliano na nidhamu katika usimamizi wa mitaji ni mambo muhimu katika kujenga imani ya wawekezaji na kuhakikisha sekta hiyo inaendelea kukua katika mazingira ya uchumi yanayobadilika duniani.

## Museveni kuzindua kampuni ya kwanza ya bima ya Kiislamu Uganda

**Rais wa Uganda Yoweri Museveni anatarajiwa kuzindua kampuni ya kwanza ya bima inayofuata misingi ya Kiislamu nchini humo, hatua inayotajwa kuwa muhimu katika kupanua huduma za kifedha na kuongeza ujumuishaji wa wananchi katika mfumo wa bima.**

**Kwa mujibu wa habari iliyochapwa katika tovuti ya Nile Post, kampuni hiyo iitwayo Tamini Insurance Company itazinduliwa rasmi Machi 3, 2026 katika viwanja vya Millennium Park, Lugogo.**

**Maafisa wanasema kampuni hiyo italeta huduma za bima zinazofuata mfumo wa takaful, ambao unategemea ushirikiano na kugawana hatari badala ya mfumo wa kawaida wa kibiashara. Chini ya mfumo huo, wanachama huchangia katika mfuko wa pamoja unaosaidia washiriki wanapopata majanga au hasara.**

**Akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari, Meneja wa Ofisi ya Mwenyekiti wa Taifa (ONC) wa tawala cha NRMM Hadijah Namyalo Uzeiye alisema mpango huo unalenga kusaidia wananchi wenye kipato cha chini na wajasiriamali wadogo kupata kinga ya kifedha.**

**Alisema kiwango cha matumizi ya bima nchini Uganda bado ni kidogo, kikiwa karibu asilimia moja pekee, hali inayowaacha wananchi wengi bila ulinzi wa kifedha wanapokumbwa na majanga. Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Tamini Insurance Mohamud Omar alisema kuanzishwa kwa kampuni hiyo ni hatua muhimu katika kukuza huduma za kifedha zinazozingatia maadili na misingi ya Shariah.**

## Wito: Utajiri wa madini Afrika uendeshe viwanda

**Mkutano wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini barani Afrika, Mining Indaba 2026, umehitimisha kwa wito kwa nchi za Afrika kuhakikisha rasilimali zao za madini zinatumika kuchochea maendeleo ya viwanda badala ya kuwanufaisha zaidi wawekezaji wa nje.**

**Ripoti na mijadala ya mkutano huo uliofanyika Cape Town, Afrika Kusini, inaonesha kuwa bara la Afrika linamiliki zaidi ya asilimia 30 ya akiba ya madini duniani, lakini linapata chini ya asilimia tano ya thamani ya mlolongo mzima wa biashara ya madini. Hali hiyo inaelezwa kuwa si tatizo la ukosefu wa maarifa, bali changamoto ya sera, usimamizi na nguvu ya majadiliano ya kiuchumi. Katika mkutano huo, viongozi na wadau wa sekta ya madini walisisitiza kuwa nchi za Afrika zinapaswa kushirikiana katika kupanga mikakati ya pamoja, hasa wakati dunia ikiingia katika uchumi unaotegemea nishati safi unaohitaji madini mengi kutoka Afrika.**

**Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2023 na 2024 Afrika ilisafirisha madini yenye thamani ya karibu dola bilioni 250, huku makadirio yakionesha kuwa ndani ya miaka 25 ijayo rasilimali za madini zenye thamani ya dola trilioni 1.6 zinaweza kuchimbwa barani humo.**

**Wataalamu wanasema ili Afrika inufaike ipasavyo, serikali zinapaswa kuimarisha usimamizi wa mapato ya madini, kufunga mianya ya upotevu wa kodi na kuanzisha mifuko ya uwekezaji au benki za maendeleo zitakazotumia mapato hayo kuendeleza viwanda barani humo.**




# Saudi Arabia, Malaysia na UAE zaongoza teknolojia ya fedha ya Kiislamu duniani

Saudi Arabia, Malaysia na Falme za Kiarabu (UAE) zinaongoza ukuaji wa teknolojia ya fedha za Kiislamu (Islamic fintech) duniani, huku sekta hiyo ikitarajiwa kufikia thamani ya miamala ya dola bilioni 341 ifikapo mwaka 2029.

Hayo yameelezwa katika ripoti mpya ya Global Islamic Fintech Report 2025/26 iliyoripotiwa na tovuti ya habari Middle East Online.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ukuaji huo unaendeshwa na mabadiliko ya haraka ya kidijitali katika huduma za fedha zinazofuata misingi ya Shariah, pamoja na sera rafiki za serikali, ubunifu wa kanuni na ongezeko la mahitaji ya huduma za kifedha zilizo na misingi ya maadili.

Ripoti inaeleza kuwa sekta ya Islamic fintech sasa imevuka hatua ya majaribio na




kuanza kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa fedha, hasa katika nchi za Ghuba na Asia ya Kusini Mashariki.

Saudi Arabia imejitokeza kama injini muhimu ya ukuaji kutokana na mageuzi ya kiuchumi yanayohusiana na mpango wa Vision 2030, pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji na leseni za benki za kidijitali.

Kwa upande wake, Malaysia inaendelea kuwa kinara kutokana na mfumo wake uliokomaa wa fedha za Kiislamu na kanuni zilizo wazi, huku UAE ikijiweka kama kitovu cha fintech kupitia sera zinazohamasisha ubunifu na ushirikiano wa kimataifa.

Kwa mujibu wa makala iliyochapishwa na Middle East Online, masoko haya matatu yanachangia sehemu kubwa ya shughuli za Islamic fintech duniani, hasa katika huduma za malipo ya kidijitali, ufadhili wa mtandao (crowdfunding), mikopo ya moja kwa moja kati ya watu na majukwaa ya uwekezaji yanayofuata Shariah.

Ripoti hiyo pia inaonyesha kuwa matumizi ya Islamic fintech yanaongezeka katika masoko mapya barani Afrika na Asia Kusini, yakisaidiwa na kuongezeka kwa matu-

## Saudi Arabia yazindua mwongozo wa kidijitali wa Umrah

**Saudi Arabia imezindua mwongozo mpya wa kidijitali unaolenga kuwasaidia mahujaji wa Umrah kufanya ibada hiyo kwa urahisi na usalama zaidi. Mpango huo umetangazwa na Wizara ya Hajj na Umrah, kwa mujibu wa ripoti ya mwandishi Sakina Fatima iliyochapishwa katika tovuti ya Siasat.com.**

**Mwongozo huo umetolewa kama sehemu ya kampeni ya "Coming to Umrah" na umetengenezwa kwa ushirikiano na mamlaka zinazohusika na usimamizi wa Misikiti Mitakatifu ya Makka na Madina pamoja na Tume ya Kifalme ya Jiji la Makka na maeneo matakatifu.**

**Kwa mujibu wa wizara hiyo, mfumo huo unalenga kuwapa raia wa Saudi Arabia na wageni taarifa muhimu kuhusu hatua za safari ya Umrah na huduma zinazopatikana katika maeneo matakatifu. Mwongozo huo unajumuisha ramani za kidijitali zinazoonyesha milango ya kuingia, sehemu za huduma na maeneo muhimu ndani ya Msikiti Mkuu wa Makka na Msikiti wa Mtume Madina.**

**Ripoti ya Siasat.com inaeleza kuwa mwongozo huo pia unaeleza hatua za ibada ya Umrah kuanzia maandalizi ya safari, kuwasili katika miji mitakatifu, hadi kukamilisha ibada. Aidha unatoa maelekezo ya afya, usafiri na namna ya kupanga ziara ili kupunguza msongamano. Mwongozo huo unapatikana katika lugha 16 za kimataifa na ni sehemu ya juhudi za Saudi Arabia kuboresha huduma kwa mahujaji na kuendeleza matumizi ya teknolojia katika sekta ya Hajj na Umrah.**

## Mahitaji elimu ya uwekezaji wa Kiislamu yaongezeka Uingereza

**Mahitaji ya mwongozo kuhusu uwekezaji u naozingatia maadili na misingi ya Kiislamu yanaongezeka ndani ya jamii ya Waislamu nchini Uingereza, wadau wakisema elimu ya fedha ni muhimu ili kusaidia watu kufanya maamuzi sahihi bila kuvunja imani zao.**

**Hoja hiyo iliibuliwa katika maonesho na mjadala wa fedha za halal uliofanyika Batley, tukio lililoripotiwa na mwandishi Sanah Akhtar katika tovuti ya Asian Standard.**

**Tukio hilo liliwaleta pamoja wanazuoni wa fedha za Kiislamu, wataalamu wa uwekezaji na viongozi wa jamii kujadili namna Waislamu wanavyoweza kushiriki katika mfumo wa kifedha wa Uingereza huku wakizingatia mafundisho ya dini.**

**Kwa mujibu wa waandaaji, moja ya changamoto kubwa inayokabili jamii ni ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu huduma za kifedha zinazokubalika Kiislamu, hasa katika masuala ya kununua nyumba, uwekezaji, mipango ya kustaafu na mirathi.**

**Mratibu wa tukio hilo, Abdul Aziz Ravat, alisema bidhaa za kifedha za Kiislamu mara nyingi zinategemea mfumo wa ushirikiano wa faida badala ya riba, jambo linalowezesha watu kuwekeza bila kukiuka misingi ya dini. "Kuna uhitaji mkubwa wa taarifa zinazofikika kirahisi ili watu waweze kufanya maamuzi sahihi yanayolingana na imani zao," alisema, akinukuliwa na Asian Standard.**

MAHMOUD NYAMGUMA

# Vizuizi vikali Ijumaa ya pili ya Ramadhan ndani ya Masjid Al Aqswa



Maelfu ya Waislamu wa Kipalestina wameswali Ijumaa ya pili ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan katika Msikiti wa Al-Aqsa chini ya vizuzi vya kuingia katika mji wa Al Quds na ulinzi mkali wa vikosi vya Israel, shirika la Arab News linaripoti.

Mashirika ya haki za binadamu yanasema Israel iliruhusu takribani Wapalestina 10,000 pekee kutoka Ukingo wa Magharibi (West Bank) kuingia kwa ajili ya ibada hiyo, idadi ndogo ikilinganishwa na mamia ya maelfu waliokuwa wakishiriki kabla ya Oktoba 7, 2023 mgogoro wa sasa ulipopamba moto.

Wanaume walio chini ya miaka 55 na wanawake chini ya miaka 50 walizuiwa, isipokuwa watoto wenye umri usiozidi miaka 12.

Waislamu hao walilazimika kukusanyika mapema katika vizuizi vya kijeshi vilivyowekwa kati ya Ukingo wa Magharibi na Jerusalem, wakipitia ukaguzi mkali wa kiusalama kabla ya kuruhusiwa kuendelea na ibada.

Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), zaidi ya vizuizi 500 vya kudumu na vya muda ikichangia changamoto za kijamii na kiuchumi kwa zaidi ya Wapalestina milioni 3 wanaoishi Ukingo wa Magharibi. Wachambuzi wanasema hatua hizi zinaathiri haki ya uhuru, ikiwemo wa kuabudu kama zilivyoainishwa katika sheria za kimataifa.

Sala hizi zimefanyika kwa mara ya kwanza tangu kuanza kutekelezwa kwa makubaliano dhaifu ya kusitisha mapigano kati ya Israel na kundi la Hamas mwezi Oktoba mwaka jana.

Tangu kuanza kwa vita vya Gaza mwaka 2023, Wizara ya Afya ya Palestina imeripoti vifo vya zaidi ya Wapalestina 72,000 katika Ukanda wa Gaza, wengi wao wakiwa wanawake na watoto, huku maelfu wengine wakijeruhiwa na miundombinu muhimu kuharibiwa vibaya. Kwa Wapalestina kurejea kuswali katika msikiti wa Al-Aqsa – eneo la tatu kwa utakatifu katika Uislamu – ni zaidi ya ibada; ni ishara ya uthabiti na mapambano ya kiimani dhidi ya wanachokiona kuwa ni uvamizi na uonevu wa muda mrefu.

## Kifo cha mkimbizi Mrohingya chaamsha hasira za Waislamu Marekani

**Baraza la Mahusiano ya Kiislamu Marekani (CAIR) limetaka uchunguzi wa haraka, huru na wa wazi wa kifo cha mkimbizi Muislamu Mrohingya, Nurul Amin Shah Alam, mwenye uoni hafifu, aliyeachwa maili kadhaa kutoka nyumbani kwake na maafisa wa ulinzi wa mipaka katika jimbo la New York.**

**Mwili wa Shah Alam ulipatikana baada ya kuripotiwa kutoweka tangu Februari 19 na kuzua maswali mazito kuhusu usalama na utu wa wakimbizi Waislamu wanaoishi Marekani, shirika la Anadolu Ajensi limeripoti.**

**Shah Alam alikuwa chini ya ulinzi akisubiri kusikilizwa kwa kesi iliyomalizika kwa kukubali kosa dogo baada ya sintofahamu ya kuingia eneo binafsi. Inadaiwa hakuelewa maagizo ya kuachia fimbo ya pazia aliyokuwa akiitumia kama msaada wa kutembelea na uoni hafifu na hakujua Kiingereza. CAIR, tawi la New York, imesema haiingii akilini kwa maafisa wa usalama kumwacha mkimbizi mwenye uoni hafifu katika eneo asilolifahamu bila kuhakikisha usalama wake. Takwimu za UNHCR zinaonesha zaidi ya Waislamu Rohingya milioni 1.1 wamekimbia mateso nchini Myanmar katika muongo uliopita, wakiwa katika mazingira hatarishi ya kiafya na kijamii, hivyo kulazimu nchi zinazowapokea kuwajibika zaidi kulinda utu na maisha yao.**

**Wakati huo huo, viongozi wa Bunge la Marekani akiwemo mwenyekiti wa Caucus ya Waasia na Wapacific, Grace Meng, wameeleza kusikitishwa na tukio hilo wakilitaja kuwa ni kushindwa kwa wajibu na utu wa msingi.**

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

# Tunapofunga Ramadhan tuwaombee waliokosa neema ya amani



Moja ya habari zilizochapishwa kwenye gazeti hili hivi karibuni, ilihusu madhila na mateso yanayoendelea kuwapata Wapalestina waishio Ukanda wa Gaza katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan.

Kwa miaka mitatu mfululizo, mwezi wa Ramadhan umekuwa mchungu kwao kutokana na uvamizi na uonevu wanaofanyiwa na utawala ghasibu wa Israel. Madhila wanayopitia Waislamu wa Gaza pia yanawakabili Waislamu wa Yemen, Libya, Sudan na wale waishio katika mji wa Rakhine nchini Myanmar na wenzao wa jimbo la Xinjiang nchini China.

Vyanzo mbalimbali vya habari ulimwenguni vinaeleza kuwa, Waislamu waishio kwenye mataifa hayo wanapitia changamoto zinazofanya utekelezaji wa ibada ya funga na nyinginezo zinazoambatana na msimu huu kuwa mgumu kwao kutokana na vita, vurugu za kijamii na kisiasa, njaa, kuteswa, kubaguliwa na kufungwa jela.

Waislamu hao, kila siku wanakufa kutokana na migogoro iliyochochewa na mataifa ya Magharibi. Kwa hiyo, katika msimu huu wa Ramadhan tuna kila sababu na haja ya kumuomba Allah awape nguvu na imani ndugu zetu hao waweze kukabiliana na ukatili unaoendelea kutekelezwa na majeshi ya nchi za Magharibi na washirika wao.

Ni vigumu kuelewa masahibu wanayoyapata Waislamu walio katika maeneo yenye vita. Vuta picha unafunga mwezi wa Ramadhan katika hali ya usalama na amani na huku unatafakari kuhusu hali tete ya vita inayowakabili Waislamu wenzako kule Gaza, Libya, Sudan, Mynamar na Yemen.

Licha ya funga ya Ramadhan kuwa ni fursa ya kusamehewa madhambi, pia funga inatufunza namna ya kujizatiti vilivyo dhidi ya changamoto za maisha ya kila siku. Si hivyo tu bali funga inatufanya tuhisi machungu na mateso yanayowasibu ndugu zetu walio vitani, ambao licha ya kuishi na wasiwasi, mashaka na hofu, pia wanakumbana na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa chakula, maji na mahitaji mengine muhimu.

Ni kwa msingi huo, tuna kila sababu ya kuwaangalia kwa jicho la huruma ndugu zetu hao wanaokabiliwa na machafuko ya kisiasa na vita huko Palestina, Iraq, Libya, Somalia, Yemen, Syria, Sudan na kwingineko.

Kwa upande mwingine, kuna mamilioni ya wakimbizi wa Kiislamu wakiwemo wanawake na watoto wakiwa wametapakaa katika nchi za Mashariki ya Kati na Ulaya wakilia kuomba msaada wa chakula, mahema, maji na sitara dhidi ya jua la mchana na baridi ya usiku.

Tusipoyatazama haya kwa makini, ulimwengu wa Kiislamu utapoteza undugu, huruma na upendo baina ya Waumini ulioelezwa na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) aliposema: "Utawaona Waumini katika kuhurumiana kwao na kupendana kwao na kushikamana kwao ni kama mwili mmoja, pindi kiungo kimoja kinapougua mwili mzima hupata taabu kwa homa na kukosa usingizi." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii ituzindue kutoka katika fikra hasi za kuamini kuwa, machafuko ya kisiasa na vita vinavyopiganwa katika ardhi za Waislamu vinawahusu Waislamu walioko katika nchi hizo pekee.

Hebu tujiulize, ni kwanini hatushtushwi na taabu na mateso yanayowapata Waislamu wenzetu huko Yemen, Iraq, Palestina, Somalia, Libya, Sudan na kwingineko kunakorindima risasi, makombora, mizinga, mabomu ya kutegwa ardhini na yale ya kudondoshwa kwa ndege vita?

Kwa kumuamini kwetu Allah Ta'ala na Mtume wake huku tukijiweka kando na mateso yanayowafika Waislamu wenzetu au hata kushiriki kusababisha mateso hayo, tunakwenda kinyume na mafundisho ya Uislamu. Nyoyo zetu zijawe na simanzi kwa kuona kwamba hatujafanya lolote kuwapunguzia makali ya mateso au hata kuwafariji ndugu zetu wanaoteseka kwa sababu ya vita.

Tunapaswa tutambue kuwa Allah hashindwi kuwanusuru wanaoteseka, lakini wajibu wa kuwasaidia na kuwanusuru kwa hali na mali ni wa kwetu sisi. Ni mara ngapi tunanukuu aya za Qur'an zinazohimiza undugu, umoja na mshikamano wa Kiislamu? Uko wapi basi undugu na umoja huo linapokuja suala la kuwahurumia Waislamu wenzetu wanaotaabika huku na kule?

Wakati tukitekeleza ibada ya swaumu, ni wajibu wetu tujiulize tumefanya nini kuhusu ndugu zetu wanaokabiliwa na mateso mbalimbali na wengine wakifa baharini kwa sababu ya kukimbia nchi zao kwenda Ulaya kwa mashua za mbao kwa sababu nchi zao zina vita na hazikaliki.

# Upunjaji mizani: jinai inayohalalishwa kimyakimya katika jamii zetu

## Tatfif katika biashara na uchumi:: Chanzo cha kuvunjika kwa uaminifu

**Qur'an katika Sura ya At-Tatfif [83:1–6] inatufundisha madhara ya upunjaji mizani: "Maangamizi yatawathibitikia wapunjao. Wale wanapojipimia kwa watu hupokea kipimo kamili, lakini wanapowapimia kwa (kipimo) cha mizani mingine wanapunguza. Je, Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa. Katika Siku iliyo kuu kabisa? Siku watakaposimama watu wote mbele ya Mola Mlezi wa walimwengu wote?"**

Upunjaji mizani ulianza kutajwa wazi katika mazingira ya biashara na ndiyo maana wengi wanapozungumzia Tatfif, fikra zao hurudi sokoni.

Hata hivyo, katika ulimwengu wa leo, biashara na uchumi vimepanuka zaidi ya mizani ya uzito (mfano: tani, kilogramu, gramu) na ujazo (lita). Upunjaji nao umevaa sura mpya ya kisheria, ya kitaasisi, na mara nyingi, ya kuheshimiwa.

Biashara inapopoteza mizani ya uadilifu, uchumi mzima hupoteza uaminifu wake.

### Tatfif sokoni na kwenye huduma

Bado upunjaji wa wazi upo katika maeneo kadhaa ikiwemo kupunguza ujazo wa bidhaa, kupandisha bei bila sababu halali na pia katika uuzaji bidhaa feki na hafifu kwa jina la ubora.

Huu ni upunjaji wa moja kwa moja unaoumiza haraka mnunuzi, lakini pia huua dhamira ya mfanyabiashara mwenyewe.

Aya za Qur'an zinatufundisha kuwa kila bidhaa iliyopunguzwa au kuuzwa kwa ujanja, huacha madhara katika jamii nzima. Mfano ni pale sokoni ambapo mfanyabiashara anapunguza uzito wa unga au ujazo wa mafuta bila taarifa, hapo, mnunuzi hupoteza fedha na huthibitisha dhana ya kutokuwepo kwa uaminifu.

### Tatfif katika mikataba na makubaliano

Tatfif (upunjaji) mkubwa zaidi hutokea kwenye makaratasi katika namna kadhaa ikiwemo mikataba inayotekelezwa nusu, masharti yanayoheshimiwa kwa upande mmoja tu, na ahadi zinazotolewa kwa maneno lakini kuvunjwa kwa vitendo.

Hapa mizani inapunjwa si kwa bidhaa, bali kwa uaminifu. Na pale uaminifu unapokosekana, biashara hugeuka kuwa vita ya ulaghai, ujanja badala ya ushirikiano. Qur'an inatufundisha kuwa mizani ya haki sio tu ya bidhaa bali pia ya maneno na matendo.

### Tatfif katika zabuni na miradi

Katika uchumi wa kisasa, tatfif huonekana pia katika miradi inayolipwa kikamilifu lakini kutekelezwa chini ya kiwango, zabuni zinazotolewa bila uadilifu, na kazi zinazopokelewa bila nia ya kutoa thamani halisi.

Matokeo yake ni miundombinu hafifu, huduma duni, na hasara kubwa kwa jamii nzima. Kwa mfano, mradi wa ujenzi uliopokea fedha kamili lakini ukakamilika kwa kiwango cha chini huacha madhara ya muda mrefu kwa jamii ambapo barabara au madarasa ya shule huharibika haraka.

### Tatfif katika mishahara na thamani ya kazi

Upunjaji hauko upande wa mwajiri pekee. Mwajiri anayelipa ujira mdogo usiolingana na kazi ni mpunjaji. Mfanyakazi anayepokea mshahara kamili bila kutoa juhudi stahiki naye ni mpunjaji. Qur'an inaweka mizani ya pande zote mbili: haki lazima iendane na wajibu.

### Athari za tatfif kwa uchumi wa jamii

Tatfif wa kiuchumi huzaa kupanda kwa gharama za maisha, kudorora kwa ubora wa bidhaa na huduma, kukosekana kwa uaminifu baina ya watu, na mwishowe, hupelekea kudumaa kwa uchumi wa taifa.

Uchumi unaokosa uadilifu hauanguki ghafla— bali taratibu, bila kelele. Qur'an inatufundisha kuwa mizani ya haki si chaguo tu bali kielelezo cha ufanisi wa jamii na baraka za kiuchumi.

Baraka na uchumi wa uadilifu

Qur'an haiahidi utajiri bila juhudi, bali inaahidi baraka kwa uadilifu. Biashara yenye mizani huenda ikaonekana ndogo, lakini hukua kwa uthabiti. Biashara yenye tatfif huweza kuonekana inafanikiwa, lakini hukosa baraka na hudumu kwa muda mfupi.

### Hitimisho na muendelezo

Tatfif katika biashara na uchumi ni chanzo cha kuvunjika kwa uaminifu wa kijamii. Na bila uaminifu, hakuna uchumi unaoweza kusimama imara.

Madhara ya tatfif hayaishii hapa. Tatfif inapopenya kwenye uongozi, siasa na utumishi wa umma, madhara yake huwa makubwa zaidi, kwa sababu huathiri maamuzi yanayogusa mamilioni ya watu.

Katika makala inayofuata, tutachunguza tatfif katika uongozi, siasa na utumishi wa umma na jinsi upunjaji wa haki na uwajibikaji unavyozaa mifumo ya dhulma na kupelekea wananchi kukata tamaa.

***Usikose makala inayofuata.***

رمضان

MAKALA
MAALUM

0712 690 811



NA SHEIKH
SEIF RUGA

SEHEMU YA
2

# Nyudhuru za kisheria zinazoruhusu kuacha kufunga Ramadhan

**Makala iliyopita iliangazia sababu za kisheria zinazoruhusu mtu kufungua swaumu ya Ramadhan, ikiwamo kusafri safari ya halali, utu uzima (ukongwe) na kuumwa. Makala ya leo ni mwendelelzo wa makala iliyopita. Sasa endelea...**

## Kikongwe, ajuza na mwenye ulemavu

Vikongwe, ajuza na wenye ulemavu wa kudumu usio na matumaini ya kupona wameruhusiwa kula mchana wa Ramadhan. Kikongwe au ajuza aliyerukwa na akili kwa sababu ya utu uzima, huyu hatofunga wala kulipa fidia.

Ama yule ambaye hajarukwa na akili atatoa fidia ya kulisha masikini mmoja kwa kila siku ya mwezi wa Ramadhan – ima kwa kutoa nafaka (kama vile mchele au unga), kiasi cha robo pishi (takriban gramu 562 au nusu na robo), au akitaka ataandaa chakula kilichopikwa na kuwalisha masikini kulingana na idadi ya siku alizofungua.

Mfano, ikiwa aliacha kufunga siku 30 atawaalika masikini 30, na kadhalika. Vikongwe na ajuza wameruhusiwa kufungua kwa kuwa hawawezi kuimudu funga. Isitoshe, katika Uislamu mtu halazimishwi kufanya jambo asiloliweza. "Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi ila kwa kadiri ya uwezo wake." [Qur'an, 2:286].

## Mgonjwa

Mgonjwa ambaye ugonjwa wake unatarajiwa kupona ameruhusiwa kufungua swaumu, lakini atalazimika kulipa siku alizofungua. Mgonjwa wa aina hii ana hali tatu: Mosi, ikiwa kufunga hakumsumbui wala hakumdhuru, basi ni lazima afunge kwa kuwa hana udhuru wa kufungua.

Pili, ikiwa kufunga kunamsumbua lakini hakumdhuru, basi ni bora afungue. Haifai kufunga kwa yule ambaye swaumu inamsumbua kwani kufanya hivyo ni kuacha ruhusa ya Allah Ta'ala na kujitaabisha nafsi bila sababu. Kadhalika, sharia ya Uislamu imejengwa juu ya urahisi na kuondoa mashaka kwa yule ambaye hana uwezo wa kufunga.

Tatu, ikiwa kufunga kunamdhuru, basi ni lazima afungue na hairuhusiwi kwake kufunga. Mgonjwa akipatwa na maradhi katikati ya siku ya Ramadhan hali ya kuwa amefunga na ikawa ni vigumu kuendelea hadi jioni, anaruhusiwa kufungua kwa kuwa udhuru umetokea na atalazimika kuilipa siku hiyo.

Vilevile, ikiwa daktari bingwa, mwadilifu na mwaminifu katika dini yake atathibitisha kwamba kufunga kutamsababishia maradhi au kuchelewa kupona, basi anaruhusiwa kufungua ili kulinda afya yake na kujiepusha na madhara, kisha atakuja kulipa siku alizokula baada ya Ramadhan kumalizika.

## Mwanamke mwenye hedhi, nifasi na mjauzito

Mwanamke mwenye hedhi au nifasi ni haramu kwake kufunga. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "...je, si kweli kwamba (mwanamke) anapopata hedhi hasali wala hafungi? Huo ndiyo upungufu wa dini yake..."

Mwanamke huyu atalazimika kulipa siku alizofungua, kwa ushahidi wa hadith ya mama Aisha (Allah amuwie radhi) ambaye aamesema: "Tulikuwa tukipata hedhi katika zama za Mtume wa Allah, tukaamrishwa kulipa swaumu wala hatukuamrishwa kulipa sala."

Iwapo damu ya hedhi itaanza kutoka hali ya kuwa amefunga, hata kama ni muda mfupi kabla ya kuzama kwa jua, swaumu ya mwanamke huyo itabatilika na atalazimika kuilipa. Na ikiwa atatwaharika katikati ya mchana wa Ramadhan, swaumu ya siku hiyo haitahesabika kwa kuwa mwanzo wa siku ulikuwa na hali inayopingana na swaumu.

Lakini akitwaharika usiku wa Ramadhan, hata kama ni muda mfupi kabla ya Alfajiri, atalazimika kufunga siku inayofuata na swaumu yake itakuwa sahihi, bila kujali kama asubuhi ameoga josho la kisharia au la. Na huu ndiyo mtazamo sahihi kwa mujibu wa kauli yenye nguvu ya wanazuoni.

Ama mwanamke mjamzito na anayenyonyesha akihofia kupata madhara yeye mwenyewe, anaruhusiwa kufungua na atakuja kuilipa siku hiyo bila ya kutoa fidia yoyote. Na ikiwa atahofia kufunga kwa ajili ya mtoto wake tu (na siyo nafsi yake), atalazimika kuilipa siku hiyo pamoja na kutoa fidia, kwa mujibu wa kauli sahihi ya wanazuoni.



# فتاوى رمضان



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

**Swali: Ni nini hukumu ya kutumia mswaki na dawa ya meno baada ya alfajiri?**

**Jibu:** Hakuna tatizo kwa mfungaji kusafisha meno yake kwa mswaki na dawa ya meno, lakini kutokana na nguvu ya dawa ya meno, haipaswi kuitumia wakati wa funga kwa sababu inaweza kupenya na kufika kooni na hatimae tumboni bila mtu kujua. Hakuna haja wala dharura ya kufanya hivyo.

Ni vema mtu akaacha kutumia dawa ya mswaki wakati wa mchana, asubiri hadi afungue, na afanye jambo hili usiku au kabla ya alfajiri, sio mchana. Lakini kwa asili, jambo hili linaruhusiwa na halina dosari.

**Swali: Ni nini hukumu ya kumeza mate kwa mtu aliye kwenye mfungo?**

**Jibu:** Haiwezekani kimaumbile kuepuka kumeza mate hivyo hakuna tatizo kumeza mate ya kawaida wakati wa kufunga. Jambo hilo haliharibu funga na hakuna tofauti ya kimtazamo kati ya wanazuoni wa Kiislamu kuhusu hili.

Lakini kama ni makohozi au mate yenye uchafu (balaghamu) yanayotoka kwenye kifua au pua ambayo yamefika mdomoni; hayo yanapaswa kutemwa na si sahihi kumeza, kwa sababu ni vitu vinavyoweza kuepukwa. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Kuna mwanaume alijamiiana na mkewe wakati wa mwezi wa Ramadhani kabla ya alfajiri, na waliendelea hadi baada ya alfajiri. Ni nini wanapaswa kufanya?**

**Jibu:** Hawa wanapaswa kutubu na kufanya kafara (fidia). Kafara ni kumuachilia huru mtu aliye mtumwa. Ikiwa hawawezi, basi wafunge miezi miwili mfululizo (siku 60). Na ikiwa kufunga pia hawawezi, basi wawalishe maskini 60, kila mmoja katika hao maskini apewe nusu pishi ya chakula cha kawaida cha eneo hilo (takriban kilo 1.5).

Zaidi ya kafara hii, kila mmoja pia anapaswa kuilipa siku hiyo ya funga ambayo walifanya tendo hilo la jimai. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

**Swali: Ni ipi hukumu ya mwanaume aliyemlazimisha mkewe kufanya naye tendo la ndoa wakati wa mchana wa Ramadhan, ikiwa hawezi kuachilia mtumwa wala kufunga kama kafara.**

**Jibu:** Ikiwa hali halisi ni kama ulivyoeleza, kafara ya tendo la ndoa lililotokea siku moja ni kuwalisha maskini 60, kila mmoja apewe nusu pishi ya chakula cha kawaida cha eneo hilo (ni sawa awe amewalisha mchana au jioni, inatosha).

Kwa upande wa pili, mke hawajibiki kulipa kafara kwa sababu alilazimishwa. Ni mwanaume binafsi ndiye anawajibika kutubu kwa Allah kutokana na kitendo hiki kisicho halali. Mwanaume pia anapaswa kufidia siku ya kufunga ambapo tendo hilo lilitokea.

Tunamuomba Allah amsamehe yeye, na atusamehe Waislamu wote. Yeye ndiye Msamehevu zaidi.

**Swali: Kuna baadhi ya wafungaji hutumia sehemu kubwa ya mchana wa Ramadhan kuangalia tamthilia za televisheni, kucheza bao, karata au drafti. Ni nini maoni ya dini kuhusu hili?**

**Jibu:** Wafungaji wanapaswa kuwa na taqwa kwa Allah katika yote wanayoyafanya na wanayoyaacha, wakizingatia maadili na mambo yanayoruhusiwa na kuharamishwa katika kila wakati.

Kuangalia filamu na programu zisizofaa ni haramu. Miongoni mwa aina ya maudhui yaliyoharamishwa na Allah ni kama kuangalia picha za uchi au za nusu-uchi, maandishi au kauli zilizoharamishwa, muziki au burudani zinazopingana na sheria ya Kiislamu na shughuli za uwongo au uwongo wa kidini.

Kila Muislamu, mfungaji, anapaswakuwamwangalifukuhusu michezo au vyombo vya burudani anavyovitumia, kwa sababu hii inaweza kuhusisha kutazama maovu au kufanya maovu na inaweza pia kusababisha ugumu wa moyo, kupoteza heshima kwa sheria ya Allah, na kuudhi nafsi. Wafungaji wanashauriwa kutumia muda wao kwa njia yenye faida, kuepuka burudani zinazoharibu utu, maadili, au kuathiri imani zao. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

رمضان

SEHEMU YA 2

# MAKALA YA AFYA

0764 101 018



DKT. Omar A. Kasuwi

Daktari Bingwa Mshauri wa magonjwa Moyo!

Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA)

# Faida ya amadhani (Swawm) kwa msingi wa sayansi na Uisilamu wenyewe.!

**Mtume alisema:**

"Funga ni kinga."

(Bukhari) Usumbufu huu ni sehemu ya mafunzo ya subira.

Matengenezo ya Seli Na Kinga ya mwili (Autophagy-self cleansing)!

Kufunga huanzisha mifumo ya ndani ya matengenezo kama- Usafishaji wa seli zilizochoka (autophagy -self cleansing) ,Uboresha mitochondria, kupunguza uchochezi mwilini na kuimarisha ulinzi wa mwili.

Kiroho, hili linafanana na utakaso wa nafsi — kuacha tabia mbaya kama mwili unavyoondoa vitu vilivyoharibika.

Kuimarika kwa Afya ya Ubongo na Hali ya Kisaikolojia -Wakati wa kufunga, mwili huzalisha (ketoni ) zinazochochea BDNF: ambazo huboresha ufanyaji kazi wa ubongo,kumbukumbu, hulinda ubongo na huongeza utulivu wa akili. Waislamu wenye kujaaliwa kufunga Ramadhani kwa Nia na ubora wake Wengi huhisi utulivu zaidi mara baada ya ramadhani kumalizika .

Mtume alisema:-

"Akifunga mmoja wenu asiwe mchafu wa maneno wala hasira; akichokozwa aseme: Mimi nimefunga."

(Bukhari na Muslim)-Hii ni mafunzo ya kudhibiti hisia jambo linalotambulika kisayansi kama udhibiti wa ubongo wa mbele (prefrontal control).Kufunga Ramadhani haiathiri tu kimetaboliki bali pia huathiri hisia na fikra.Tafiti za Ramadhani zinaonyesha:,kuongezeka kwa ubora wa maisha, kupungua kwa msongo na huzuni. Ketoni hutoa nishati thabiti kwa ubongo, ndiyo maana watu wengi huhisi akili kuwa wazi zaidi katikati ya Ramadhani.

Kupungua kwa Uzito na Mafuta ya Tumbo!

Kufunga Ramadhani si lazima kupunguze uzito sana, lakini huboresha muundo wa mwili.Tafiti zinaonyesha:,kupungua kwa mafuta ya mwili,hupunguza uzito endapo tu tutafunga kwa nia na kufturu kwa nidhamu ya Afya.Muhimu zaidi ni kupungua kwa mafuta ya ndani ya tumbo (visceral fat) ambayo yanahusishwa sana na ugonjwa wa moyo na kansa.

Usawazishaji wa Homoni za Njaa!

Kufunga hubadilisha mabadiliko makubwa ya homoni za ghrelin , na leptin .Hali hii husababisha kupungua kwa homoni hizi hatimae kupunguza hamu ya kula na kupunguza kula bila mpangilio, Kadri Siku za Funga zinavoendelea mwili ndivo unavozidi kujiimarisha sehemu zote. Homoni hizi hupungua na kupunguza kuskia njaa na hamu ya kula pia ,pamoja na kwamba Mfungaji huendelea kujishughulisha na majukumu yake ya kila siku ya kujipatia rizki. Ndiyo maana mwishoni mwa Ramadhani mtu huwa haisi njaa kuliko mwanzoni.

Kutokunywa maji mchana husababisha upungufu mdogo wa maji kwa muda na mwili hujirekebisha kuhifadhi maji yanayozalishwa ndani, ili kuiweka hali ya damu katika usawa unaotarajiwa ,kwa kuzuia mkojo kipindi hiki cha kufunga,

Wakati wa kufungua -Njia bora:ni kuanza na Maji kiasi,Tende na baadae mle chakula laini kwanza, kwa kufuatiwa na kile kiasi laini kiasi kigumu. Si afya kuftari kwa wingi kwani kuna athiri afya zenu. Kwa ubora zaidi tuftari chakula chenye uwiano sahihi wa Protein, Wanga, mafuta na vitamini.

Mazoezi-Mazoezi mepesi baada ya futari husaidia mwili kutumia sukari vizuri na Mazoezi bora zaidi ni kutembea kwenda kuswali msikitini swala ya tarweh.

faida za funga kwa msingi wa Iman.!

Sayansi inaeleza jinsi kufunga kunavyosaidia mwili.

Uislamu unaeleza dhumuni lake."Enyi mlioamini! Mmefaradhishiwa kufunga kama walivyofaradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu."

(Qur'an 2:183)Hivyo lengo si njaa — ni taqwa, yaani ulinganifu wa Allah katika maisha yote.

Nidhamu ya tabia na kujidhibiti!

Mtume amesema:"Funga ni ngao."

(Bukhari na Muslim) Ngao dhidi ya:hasira,maneno mabaya,tabia mbaya

Na pia:"Asiyeacha kusema uongo na kuutenda, Mwenyezi Mungu hana haja na kuacha kwake chakula na kinywaji."

(Bukhari)Hivyo kufunga hubadilisha tabia, si tumbo pekee.

Msamaha na mwanzo mpya- "Atakayefunga Ramadhani kwa imani na kutaraji thawabu atasamehewa madhambi yake yaliyopita."

(Bukhari na Muslim)Ramadhani ni utakaso wa moyo kama mwili unavyosafishwa.

Ikhlasi-ibada ya siri-"Kila amali ya mwanaadamu ni yake isipokuwa kufunga — ni Yangu nami ndiye ninalipa."

(Hadith Qudsi)-Hakuna ajuaye umefunga isipokuwa Mwenyezi Mungu — hapa ndipo ukweli wa ndani hujengwa.

Huruma , Unyenyekevu ,sadaka na shukrani!

Njaa humfanya mtu atambue wenye huhitaji kwani inamkumbusha ile hali ya wale wenye kukosa kila siku katika maisha yetu.

"...ili mpate kushukuru."

(Qur'an 2:185)Kukosa kwa muda hufundisha kuthamini ulichonacho.

Hitimisho!

Funga Ramadhani si ibada pekee

رمضان

# TUJIFUNZE AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama




## Je, AI ni msaidizi au mbadala wa mwanadamu?

Akili mnemba (Artificial Intelligence – AI) imeanza kubadilisha namna watu wanavyofanya kazi duniani. Kutoka kwenye biashara hadi elimu, teknolojia hii sasa inaandika barua pepe, inachambua taarifa, inapanga ratiba na hata kujibu maswali ya wateja. Mabadiliko haya yamezua mjadala mkubwa: je, AI inakuja kusaidia binadamu au kuchukua nafasi yake?

Kwa watu wengi, jibu linaonekana kuwa katikati ya mambo hayo mawili.

### Uwezo wa AI katika kazi za kila siku

Hakuna shaka kuwa AI imeleta urahisi mkubwa katika kazi nyingi. Programu za kisasa zinaweza kuandaa rasimu za makala, kufupisha mikutano mirefu, kupanga taarifa nyingi kwa muda mfupi na kutoa majibu ya haraka kwa wateja.

Kwa upande wa biashara, hili ni jambo muhimu. Mfumo wa AI unaweza kufanya kazi saa 24 bila kuchoka. Hii ina maana kwamba maswali ya wateja yanaweza kujibiwa muda wowote, na taarifa zinaweza kuchakatwa kwa kasi kuliko binadamu. Kwa kazi zinazojirudia mara kwa mara, AI mara nyingi huwa na ufanisi mkubwa kuliko mtu.

### Mipaka ya AI ambayo bado ipo

Pamoja na uwezo huo, teknolojia hii bado ina mipaka kadhaa. AI inaweza kuchakata data, lakini haina hisia wala uzoefu wa kibinadamu. Haiwezi kuelewa kikamilifu hali ya mtu, mazingira ya kijamii, au athari za maamuzi kwa muda mrefu.

Kwa mfano, kujenga uhusiano na mteja, kuongoza timu ya wafanyakazi, au kufanya maamuzi magumu ya kimkakati bado kunahitaji akili ya binadamu. Hapa ndipo tofauti kati ya mashine na mwanadamu inaonekana wazi.

Kwa ujumla, wataalamu wa teknolojia hugawanya mifumo hii katika makundi mawili makuu: AI kama wakala na AI kama wasaidizi.

### AI kama "wakala"

Katika matumizi ya kisasa, kuna mifumo ya AI inayofanya kazi kama wakala. Hizi ni programu zinazoweza kufanya kazi kwa kiwango kikubwa bila kusubiri maelekezo ya kila hatua kutoka kwa binadamu (autopilot agent).

Mfano wake ni roboti wanaoshughulika na maelfu ya maswali ya wateja kwa wakati mmoja, au mifumo inayochambua soko la fedha na kufanya maamuzi ya haraka ya uwekezaji. Katika mazingira yenye taratibu zilizo wazi na data nyingi, wakala wa AI wanaweza kufanya kazi kwa kasi na ufanisi mkubwa.

### AI kama "wasaidizi"

Aina nyingine ya teknolojia ni AI wanaofanya kazi kama wasaidizi. Hawa hawakusudiwi kuchukua nafasi ya mtu, bali hukusudiwa kumsaidia mtu kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Programu kama ChatGPT, mifumo ya uchambuzi wa masoko, au zana zinazosaidia kupanga kazi huangukia katika kundi hili. Zinatoa mawazo, zinafupisha taarifa, na kusaidia watu kufanya maamuzi kwa taarifa sahihi zaidi. Lakini uamuzi wa mwisho hubaki kwa binadamu.

Kwa lugha rahisi, wasaidizi wa AI ni kama mshirika wa kazi anayeharakisha shughuli zako.

### Ushirikiano kati ya binadamu na AI

Uzoefu wa taasisi nyingi unaonyesha kuwa matokeo bora hupatikana pale binadamu na AI wanapofanya kazi pamoja. AI inaweza kushughulikia kazi zinazochukua muda mwingi, huku binadamu akibaki na majukumu yanayohitaji ubunifu, uamuzi na mawasiliano.

Katika ofisi nyingi leo, mtu anaweza kutumia AI kuandaa rasimu ya taarifa au kuchambua takwimu, kisha yeye mwenyewe akaiboresha, akaamua mwelekeo na kuwasiliana na watu wanaohusika. Hii inaonyesha kuwa teknolojia haiondoi nafasi ya binadamu; inaibadilisha.

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 2



# SIMULIZI YA AKINA THAMOUD WATU WA NABII SWALEH

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Tulijifunza katika toleo lililopita namna kina Thamoud walivyolewa na starehe na walivyozama katika maasi, yakiongozwa na kibri na ushirikina wa kuabudu masanamu waliyoyatengeneza wenyewe. Ndio hapo Allah akamtoa miongoni mwao mjumbe aliyeitwa Swaleh, awatoe gizani na kuwapeleka kwenye nuru.**

**Vipaumbele vya da'wa ya Mtume Swaleh (amani ya Allah imshukie) ilikuwa ni vile vile vya Mitume wengine, navyo ni Tawhid, vikiongozwa na Imani juu ya uwepo Allah, Muumba wa kila kitu mneemeshaji, anayestahiki kuabudiwa na kushukuriwa.**

**Kipaumbele kingine ni imani juu ya maisha ya akhera, yaani watu kufufuliwa, kuhesabiwa na kulipwa kwa mujibu wa matendo yao. Huko akhera, wema kuingizwa katika bustani takatifu, humo watakuta kila linaloburudisha nyoyo, macho na viwiliwili vyao. Waovu kuingizwa katika maisha ya milele motoni, humo watakutana na kila aina ya adhabu ya kuwaumiza. Tunamuomba Allah atuhifadhi waja wake.**

### Upinzani wa Thamoud

Kama walivyofanya kina Adi kwa Mtume wao Hud, wakuu (waheshimiwa) wa kina Thamoud walikaidi mafundisho ya Mtume wao, wakamkejeli, kumdhihaki na kumcheka.

Walihoji iweje mtu masikini asiye na majumba na mashamba anakuwa mtume? "Wakasema, 'Oh! Tumfuate mtu mmoja miongoni mwetu! Kwa hakika tutakuwa katika upotofu vichaa. Oh! Ameteremshiwa yeye tu ukumbusho baina yetu, bali yeye muongo na mwenye kujiona." Allah akasema: "Watakuja kujua kesho yupi muongo ajionae'" [Qur'an, 54:24-27].

Alipozidi kuwaonya na adhabu ya Allah, watu wake walimwambia: "Wewe Saleh, ulikuwa kijana mwema. Tulikuwa tunakutegemea utakuwa miongoni mwa watu muhimu katika jamii yako! Umetuvunja moyo na kutupotezea matumaini yetu kwako!" Qur'an inasema: "Wakasema, 'Ewe Swaleh, kwa hakika ulikuwa wa kutarajiwa (sana) kwetu kabla ya haya (sasa umeharibika). Unatukataza kuabudu waliowaabudu baba zetu? Na hakika sisi tuko (katika nyoyo) na shaka kwa haya unayotuitia." [Qur'an,11:62].

Na alipowapitia wakiwa kwenye barza zao, walioneshana kwa vidole vyao na kutoa maneno ya kejeli wakisema: "Mungu amsaidie baba Swaleh, maskini! mwanawe ameharika (amepotea)."

Mtume Swaleh aliyasikia maneno yao, akaona namna watu wake walivyozama katika kuipenda dunia na starehe zake, na akawasikitikia sana.

### Wakuu kuwazuia wanyonge kumuamini Swaleh

Wakuu na matajiri wa jamii ya Mtume Swaleh walipowaona watu wameanza kumsikiliza waliwakataza. Qur'an inasema: "Na wakubwa katika watu wake waliokufuru na kukadhibisha makutano ya akhera na ambao tuliwatajirisha katika maisha ya dunia walisema, 'Hakuwa huyu ila mtu kama nyinyi, anakula katika vile mnavyokula, na anakunywa katika vile mnavyokunywa. Na kama mkimtii mtu kama nyinyi, mtakuwa wenye kupata khasara. Anakuahidini ya kwamba mtakapokufa na mkawa udongo na mifupa kuwa mtatolewa (mtafufuliwa)? Hayawi hayawi haya mnayoahidiwa, hakuna (mengine) ila maisha haya ya dunia, tunakufa na kuishi, wala sisi si wenye kufufuliwa'" [Qur'an, 23:33-37].

### Mazingatio

Huu unaitwa "ushetwani" ufanywao na wakuu wa jamii pale wanapojitokeza wanaolingania watu katika dini ya Allah. Ni husda itokayo ndani ya nyoyo zao, pale wanapowaona wengine wana hamu ya kuijua na kuifuata njia (dini) ya haki.

Kuwazuia watu kuijua na kuifuata haki ni jarima (kosa) kubwa mbele ya Allah. Kwani hilo ni jambo la khiari ya moyo.

Mtu anapokataa ukweli kisha akawazuia wengine wasiukubali, anafananishwa na joka la mdimu kwenye mto. Watu huogopa hata kusogelea, wala joka nalo halina shida ya ndimu wala kuteka maji! Hii ni dhambi kubwa kwa kweli.

Mwenyezi Mungu anawaelezea watu kama hawa: "Hakika waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuia (watu kuamini) njia ya Allah, basi watazitoa kisha majuto yatakuwa juu yao, kisha watashindwa, na wale waliodumu juu ya ukafiri watakusanywa katika Jahannam." [Qur'an, 8:36].

Na katika sura nyengine, Allah anasema: "Wakasema wakuu wa kaumu yake waliotakabari kuwaambia wale walio dhaifu, wenye kuamini miongoni mwao, 'Je mnaitakidi ya kwamba Swaleh ametumwa (amepewa utume) na Mola wake?' Wakasema, 'Hakika sisi tunaamini yote aliyotumwa kuyafikisha.' Wakasema waliotakabari, 'Sisi tunayakataa yote mnayoyaamini.'" [Qur'an, 7:75-76].

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Njia 6 za kunufaika na mwezi wa Ramadhan

Hakika Allah Mtukufu ameutukuza mwezi wa Ramadhan kuliko miezi yote kwa hekima anayoijua yeye. Pengine, hekima hiyo ni kuufanya mwezi huu kuwa ni fursa adhimu kwa waja ya kupata rehema, radhi na msamaha wake.

Kuna mambo kadhaa yanayoufanya mwezi wa Ramadhan kuwa bora kuliko miezi yote, hivyo Waislamu wanatakiwa kutumia fursa ya mwezi huu kutafuta thawabu kutoka kwa Allah. Moja ya sababu hizo ni Qur'an kuteremshwa ndani ya mwezi huu katika usiku ulio bora zaidi kuliko miezi elfu moja, nao ni usiku wa cheo (Al–Qadr).

Allah anasema: "Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni uongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uongofu na upambanuzi. Basi atakayekuwa mjini katika mwezi huu na afunge. Na yule ambaye ni mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku nyingine. Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito, na mtimize hiyo hesabu, na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru." [Qur'an, 2:185].

Hebu sasa tuangalie njia (maeneo) sita ambazo Muislamu anaweza kuzitumia ili kunufaika na mwezi huu Mtukufu.

## Mosi, kukithirisha kusoma Qur'an

Ramadhan ni mwezi wa Qur'an, kama alivyosema Allah Aliyetukuka: "Mwezi wa Ramadhan ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa ni uongofu kwa watu..." [Qur'an, 2:185].

Ibn Abbas (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema makusudio ya aya hii ni kuwa, Qur'an ilianza kuteremshwa kwa Mtume katika mwezi wa Ramadham ndani ya usiku wa Laylatul Qadr. Hivyo basi, ni juu yetu kufanya juhudi katika mwezi huu kukithirisha kusoma Qur'an.

## Pili, subira

Subira ni katika ibada ngumu mno. Hawi na subira ila mchamungu na aliye mnyenyekevu kwa Allah. Swaumu inahitaji subira katika



kujizuia kula, kunywa, kujamiiana na mkeo/mumeo, na matamanio mengine. Hivyo, swaumu imetajwa kuwa ni nusu ya subira na subira malipo yake ni Pepo.

Kuhusu umuhimu wa subira, Qur'an inasema: "Na ombeni msaada kwa kusubiri na kusali, na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu." [Qur'an, 2:45]. Na huko Akhera waliosubiri wataambiwa: "Amani iwe juu yenu kwa vile mlivyovumilia, (haya ingieni katika Pepo hiyo), ni nyumba bora kabisa." [Qur'an, 13:24].

## Tatu, kuyaepuka maovu

Imekuja katika hadith kuwa, Mtume (rehema na amani ya Allah imshushie) amesema: "Ramadhan inapoingia inafunguliwa milango ya Pepo na hufungwa milango ya Moto, na mashetani (wakaidi) wanafungwa minyororo." [Bukhari na Muslim]. Ni kwa ajili hiyo utaona mwezi huu watu wengi wanajitahidi kuepuka maasi na wanajaa misikitini kwa sababu mashetani wamefungwa.

Shetani, licha ya uasi wake, anauogopa mwezi wa Ramadhan. Katika mwezi huu, vitimbi vya shetani vinakuwa dhaifu, ndiyo maana watu wengi hubadilika kitabia, wanasali na kufanya kheri mbalimbali. Ikimalizika Ramadhan, kwa kuwa mashetani huachiwa huru, watu wengi huacha kusali kana kwamba Allah yupo katika mwezi wa Ramadhan tu. Huu ni msiba ndugu zangu Waislamu. Allah asitujaalie katika hao.

## Nne, kuzidisha kuomba dua

Dua ni ibada na silaha kubwa kwa muumini. Mwezi wa Ramadhan ni fursa adhimu kwa mfungaji kutumia muda wake katika kumuomba Allah yale anayohitaji katika dunia na Akhera.

Allah anasema: "Na waja wangu watakapokuuliza habari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi ili wapate kuongoka." [Qur'an, 2:186]. "Na Mola wenu Mlezi anasema, 'Niombeni nitakuitikieni..." [Qur'an, 40:60].

Na katika hadith iliyonukuliwa na Imam Tirmidhi kuhusu watu ambao hazirejeshwi dua zao akataja ndani yake mfungaji mpaka/wakati anapofuturu. Hivyo hii ni fursa nzuri kwa mfungaji kujitahidi na kukithirisha kumuomba Allah, kwani milango ya Pepo ipo wazi na milango ya Moto imefungwa.

Masahaba wa Mtume (Allah awaridhie) walikuwa wakisema: "Tulikuwa tukiandaa kwa ajili ya Ramadhan dua maalumu ambazo tulikuwa tukizirudia/kariri kwa mwezi mzima. Tunaapa kwa Allah inakwisha Ramadhan kisha haiji Ramadhan nyingine isipokuwa Allah ametujibu yale tuliyomuomba."

## Tano, sadaka

Kutoa zaka/sadaka ni mojawapo ya aina kubwa zaidi ya wema kwa masikini na wanyonge. Katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan, sadaka/ zaka hukamilisha mahitaji muhimu ya futari na daku kwa masikini na wasiojiweza na hivyo kuwaondolea udhalili wa kuombaomba na kutamani vilivyo mikononi mwa watu. Kwa kutoa sadaka/ zaka nyuso zao husitirika, nafsi zao huenziwa, na heshima yao hulindwa.

## Sita, usiku wa cheo

Katika mwezi huu kuna usiku wa Laylatul Qadr ambao ni bora kuliko miezi elfu moja, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: "Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'an katika Laylatul Qadri, Usiku wa Cheo Kitukufu. Na nini kitachokujulisha nini Laylatul Qadri? Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu." [Qur'an, 97:1–3].

رمضان

# MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Hivi ndivyo Mtume alivyosali usiku

**Hudhayfa bin Al–Yamaan (Allah amridhie) amehadithia kuwa, usiku mmoja alisali na Mtume wa Allah (rehema za Allah na amani zimshukie), Mtume akasoma Suratul Baqara. Hudhaifa akasema moyoni mwake: "(Mtume) atarukuu baada ya kusoma aya mia moja."**

## Lakini Mtume akaendelea kusoma Suratul Baqara.

Hudhayfa akahisi kuwa huenda Mtume ataimaliza ndani ya rakaa mbili, lakini akaendelea kusoma. Mtume alisoma Suratul Baqara yote, na alipoimaliza akaanza kusoma Suratun–Nisai. Kisha akasoma Suratul Imran polepole (kwa kuzingatia hukumu na kanuni za usomaji), na kila aliposoma aya inayozungumzia utukufu wa Allah alimsabihi Allah 'Azza Wajallah' na aliposoma aya zenye maombezi (dua) alikuwa akiomba, na aliposoma aya za kujilinda (na shari) alimuomba Allah ulinzi. Kisha akarukuu na kusema: "Subhaana Rabbiyal–adhwiim." [Muslim].

Na imepokewa katika riwaya nyingine kutoka kwa Malik al–Ashja'iy (Allah amridhie) kwamba, Hudhayfa bin Al–Yamaan alisali na Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie), Mtume akasoma Suratul Baqara, akawa hapiti aya inayoelezea rehema za Allah isipokuwa anasimama na kuomba, na hapiti aya inayozungumzia adhabu isipokuwa anasimama na kuomba hifadhi (ulinzi) wa Allah.

Kisha Mtume akarukuu kiasi cha urefu wa kisimamo chake na kuomba: "Sub–haana dhiljabaruuti, wal–malakuuti, wal–kibriyaa, wal–adhamati (Ametakasika Mwenye Utawala wa kufanya atakalo, na Ufalme, na Ukubwa, na Utukufu), kisha akasujudu kwa muda mrefu mithili ya kisimamo cha kwanza huku akitamka maneno yaleyale aliyoyasema kwenye rukuu. Baada ya kusujudu, Mtume alisimama kuendelea na rakaa ya pili, akasoma Suratul Imran na sura nyingine." [Abu Daudi na An–Nasai].

## Mafundisho ya tukio hili

Imam Nawawi (Allah amrehemu) amenukuu maneno ya Imam Shafii yasemayo: "Ni Sunna kwa mwenye kusoma Qur'an ndani na nje ya sala anaposoma aya inayoelezea rehema, aombe rehema za Allah, na anaposoma aya inayozungumzia adhabu aombe ulinzi kutoka kwa Allah, na anaposoma aya inayomtukuza Allah, amsabihi (amtakase) Allah."

Jambo hili linamhusu Imam, maamuma na Muislamu yeyote – iwe ndani au nje ya sala. Na hii ndiyo rai ya wanazuoni wengi wema waliopita na waliokuja baada yao (Allah awarehemu).

## Urefu wa kisimamo cha Mtume

Imethibiti katika hadith sahihi kwamba Salamah bin Abdirrahman (Allah amrehemu) alimuuliza mama Aisha (Allah amuwie radhi): "Kisimamo (sala) cha Mtume kilikuwaje wakati wa usiku?"

Mama Aisha akasema: "Hajapata kuzidisha katika Ramadhan wala miezi mingine zaidi ya rakaa 11, akisali rakaa nne, wala usiulize uzuri wake na urefu wake (zilikuwa ndefu na nzuri sana), kisha anasali rakaa nne, wala usiulize uzuri wake na urefu wake, kisha anasali rakaa tatu."

Mama Aisha akamuuliza Mtume: "Ewe mjumbe wa Allah! Unalala kabla ya kusali witri." Mtume akamwambia: "Macho yangu yanalala lakini moyo wangu haulali." [Bukhari na Muslim]. Mama Aisha (Allah amuwie radhi) amezitaja sala za tahajjud, tarawehe na witri kuwa ni kisimamo cha usiku (Qiyaamul Layl) kwa sababu zinasaliwa wakati wa usiku pekee.

Na imekuja hadith nyingine kutoka kwa mama Aisha (Allah amuwie radhi) akisema, Mtume alikuwa akisali usiku rakaa 10, na anamalizia witri kwa kusali rakaa moja, na alikuwa akisali rakaa mbili za Sunna ya Alfajiri. Kwa hiyo alikuwa anasali rakaa 13, [Bukhari na Muslim].

Pia Imam Shaabiy amesimulia kutoka kwa Ibn Abbas na Abdallah bin Umar (Allah awaridhie wote) kuhusiana na kisimamo cha Mtume akisema, rakaa 13 alizokuwa akisali Mtume, tatu zilikuwa za witiri na mbili za Sunna ya Alfajiri.

Saikolojia
Kwa nini wat
wanapokuwa

## Uwepesi wa rakaa mbili za mwanzo

Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie) amesema: "Mmoja wenu atakaposimama usiku kwa ajili ya sala, basi afungue (aanze) sala yake kwa rakaa mbili nyepesi." [Muslim].

## Himizo la kisimamo cha Ramadhan

Tarawehe ni miongoni mwa sala za Sunna ambazo Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ametuhimiza kuzisali ndani ya mwezi wa Ramadhan. Visimamo vya usiku ikiwamo tarawehe ni darasa muhimu katika kukuza imani ya Muislamu na kuutakasa moyo kutokana na maasi, chuki, hasadi na kadhalika.

Mtume amesema: "Mwenye kusimama (kwa ajili ya sala) usiku wa Ramadhan kwa imani na kutaraji malipo kwa Allah atasamehewa madhambi yake yaliyopita." [Bukhari na Muslim]. Kutokana na hadith hii, tunapata ushahidi mwingine kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa akikithirisha kufanya ibada katika usiku wa Ramadhan.

## Kusali jamaa

Imekuja katika Masail Abi Daudi kuwa, Ahmad Ibn Hambal (Allah amrehemu) aliulizwa: "Kipi kinakupendeza zaidi? Unapenda mtu aswali na watu (tarawehe) ndani ya Ramadhan au aswali peke yake?" Akasema: "Napenda mtu aswali na watu. Napenda sana mtu aswali tarawehe pamoja na witri nyuma ya Imam, kwani Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: 'Atakayesimama (kusali) na Imam hadi amalize ataandikiwa (fadhila za) Qiyamu Llayl.'" [Tirmidhi].

JUNAYNAT ALLY DAMA



# Tusilazimishe ndoto zetu kwa watoto

Miaka ya hivi karibuni nchini India kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu matarajio ya wazazi kwa watoto—hasa pale wazazi wanapopendelea fani chache zinazoonekana kuwa "salama" na zenye hadhi, kama udaktari, uhandisi au sheria.

Kwa mujibu wa makala moja iliyochapishwa katika tovuti ya India Today, shinikizo la familia na jamii mara nyingi hujengwa juu ya dhana kwamba mustakabali mzuri una njia moja tu: ufaulu wa masomo unaoishia kwenye taaluma "zinazokubalika." Hali hii imefanya vijana wengi kuishi maisha ya kulinda ndoto za wengine badala ya kujenga mwelekeo unaoendana na vipawa vyao.

Hoja kama hiyo pia imeelezwa katika makala ya The Times of India, ikionya kwamba matarajio ya wazazi yanaweza kugeuka mzigo pale mafanikio yanapopimwa kwa jina la taaluma, si kwa uwezo halisi wa mtoto. Na katika mijadala ya mitandaoni kama Quora, hoja inayojirudia ni hii: baadhi ya wazazi hawamsukumi tu mtoto "afanya vizuri," bali wanamsukuma afanye vizuri ili afike mahali walipokwishaamua wao—mahali ambapo, mara nyingi, mtoto mwenyewe hakupata nafasi ya kusema kama anataka au la.

Ukiangalia kwa makini, hilo ndilo tatizo tunalopaswa kulizungumzia: si bidii ya mtoto kwa ujumla, bali pale mzazi anapomchagulia mtoto maisha—fani na kazi—kana kwamba mtoto ni mradi wa kukamilisha, si nafsi inayokua.

Kwa mbali sana, simulizi hizi zinafanana na hali inayotokea katika familia nyingi duniani—ikiwemo zetu. Wazazi tuna ndoto kubwa kwa watoto wetu. Tunataka wafanikiwe. Tunataka wawe na maisha mazuri kuliko yetu. Ndiyo maana mara nyingi mzazi husema kwa kujiamini: "Mwanangu atakuwa daktari," au "Lazima awe injinia."

Sababu zake ni nyingi. Wengine wanaamini fani fulani zina kipato kikubwa na hadhi isiyotetereka. Wengine wanajaribu kufuta hofu ya umasikini kwa kuwapa watoto "tiketi" ya ajira. Wengine, kwa unyenyekevu au kwa kujisitiri, wanaishi ndoto walizoshindwa kuzitimiza kupitia watoto. Wengine wanapenda tu kauli ya kujivunia mbele ya jamii: mwanangu daktari, injinia, mhasibu, mhadhiri. Lakini katika harakati hizi zote, kuna swali moja muhimu: mtoto mwenyewe anataka nini?

Na hata kabla ya hilo, je tumewahi kujiuliza Allah amempa mtoto wetu kipawa gani?

Kila mtoto ameumbwa tofauti. Wapo wanaopenda sayansi na maabara; wapo wabunifu wa sanaa, teknolojia au uandishi; wapo wanaochanua kwenye biashara, ufundi, uongozi, michezo, au kazi za kijamii. Tatizo linaanza pale mzazi anapoamua maisha ya mtoto mapema sana bila kuangalia uwezo wake wa asili—halafu anatumia mamlaka ya mzazi "kufunga" njia moja na kuzifunga njia nyingine zote.

Hapa ndipo tunapaswa kuwa wakweli. Unaweza kufanikisha kumuingiza mtoto katika fani uitakayo. Unaweza kutumia hofu, shinikizo la maneno, aibu, kulinganisha na watoto wa watu, au zawadi na vitisho. Unaweza hata kumpeleka kwenye kozi asiyoipenda na akamaliza. Lakini lazima ujiulize: kwa gharama gani?

Je, ni kwa kuua vipaji vyake halisi? Je, ni kwa kumkosesha furaha ya kufanya kile anachokipenda? Je, ni kwa kumfanya aishi maisha uliyoyatamani wewe? Maisha yako tayari umeyaishi—lakini yake atamwachia nani ayaishi? Na je, ataweza kujivunia chaguo hilo hata pale usipokuwepo, au ataishi na hisia ya "nilikamilisha ndoto ya baba/mama" bila kutimiza yake?

Tukimlazimisha mtoto kubeba ndoto zetu, mara nyingi tunaunda kizazi cha watu wanaofanana kwa vyeti lakini hawajitambui. Wanaweza kuwa na taaluma "nzuri" kwa macho ya jamii, lakini ndani wakawa hawana shauku, hawana ubunifu, na hawana maana binafsi. Wengine huishia kubadili taaluma kwa siri baada ya miaka, wengine hukwama kazini bila motisha, na wengine huanza kuichukia elimu yenyewe kwa sababu waliinusa kama kifungo.

UKHTI FATIMA SS

# Saikolojia ya kundi: Kwa nini watu hubadilika wanapokuwa kwenye umati

Na mara nyingi huanza kwa tukio dogo tu. Watu hukusanyika kwa sababu ya hasira, huzuni, au shauku ya pamoja. Dakika chache baadaye, umati huo unaweza kuwa na nguvu mpya—wakipiga kelele, kuvunja mali, au kufanya mambo ambayo wengi wao wangeona hayafai na wasingeweza kuyafanya wakiwa peke yao. Hapa ndipo wanasaikolojia huzungumza kuhusu saikolojia ya kundi au mob mentality.

Kwa ufupi, saikolojia ya kundi ni hali ambapo tabia na maamuzi ya mtu binafsi yanaanza kuongozwa na nguvu ya kundi. Mtu anayekuwa mpole na mwenye tahadhari akiwa peke yake anaweza kufanya vitendo vya haraka au vya vurugu akiwa ndani ya umati. Watafiti wa saikolojia ya kijamii wanasema hali hii hutokea pale utambulisho wa mtu unapoyeyuka ndani ya utambulisho wa kundi.

## Kundi lina nguvu ya kubadilisha tabia

Moja ya majaribio maarufu katika saikolojia yalifanywa miaka ya 1950 na mwanasaikolojia Solomon Asch. Katika jaribio hilo, mshiriki aliwekwa katika chumba na watu wengine ambao walikuwa sehemu ya utafiti bila yeye kujua. Wote waliulizwa kuchagua mstari uliokuwa sawa na mwingine. Jibu lilikuwa wazi, lakini wale washirika wa utafiti walitoa jibu lisilo sahihi kwa makusudi.

Cha kushangaza ni kwamba takribani theluthi moja ya washiriki halisi waliiga jibu lile lile lisilo sahihi. Sababu haikuwa ujinga, bali shinikizo la kijamii. Watu wengi hupendelea kufanana na kundi badala ya kusimama peke yao.

Hapa ndipo msingi wa saikolojia ya kundi unapojitokeza: binadamu ni viumbe wa kijamii. Mara nyingi tunatafuta kukubalika kuliko kuwa sahihi.

## Nini hutokea ndani ya akili ya umati

Watafiti wamebaini michakato kadhaa ya kisaikolojia inayofanya makundi kuwa na nguvu kubwa juu ya tabia za watu.

Kwanza ni kupotea kwa utambulisho binafsi (deindividuation). Katika kundi kubwa, mtu anahisi haonekani kama mtu mmoja mmoja bali sehemu ya umati. Hii hupunguza aibu, hofu ya hukumu, na hata dhamira ya kibinafsi.

Pili ni kusambaa kwa uwajibikaji. Watu wanapokuwa wengi, kila mmoja huhisi kwamba si yeye binafsi anayewajibika kwa kile kinachotokea. Hali hii inaweza kumfanya mtu kufanya jambo ambalo asingelifanya akiwa peke yake.

Tatu ni maambukizi ya hisia. Hasira, hofu, au msisimko vinaweza kusambaa haraka ndani ya kundi kama moto wa nyika. Ukiona watu wanaokuzunguka wamekasirika, kuna uwezekano mkubwa nawe ukaanza kuhisi vivyo hivyo hata kama mwanzoni hukukasirika.

Nne ni kuiga tabia za wengine. Wanadamu wana tabia ya kuiga. Ndani ya kundi, mtu mmoja akianza kitendo—kama kupiga kelele au kurusha kitu—wengine wanaweza kufuata bila kufikiria sana kuhusu usahihi wa jambo husika.

## Wakati kundi linapokuwa hatari

Si kila kundi ni tatizo. Maelfu ya watu hukusanyika katika ibada, michezo, au sherehe bila matatizo. Lakini mazingira fulani yanaweza kubadilisha mkusanyiko wa watu kuwa umati wenye vurugu.

Moja ni pale watu wanapohisi wameonewa au kupuuzwa. Hasira iliyojikusanya kwa muda mrefu inaweza kulipuka haraka. Sababu nyingine ni hali ya msongo wa kiuchumi, migogoro ya kisiasa, au propaganda zinazowafanya watu wahisi kuwa wako kwenye mapambano.

Uongozi pia una nafasi muhimu. Kiongozi mwenye mvuto anaweza kuchochea hisia za kundi na kulipa mwelekeo. Wakati mwingine hata mtu asiye na cheo rasmi anaweza kujitokeza ghafla na kuwa sauti ya umati na watu wakamfuata.

Mazingira ya tukio nayo yanaweza kuchochea hali hiyo. Maeneo yenye msongamano mkubwa, joto kali, au sehemu zenye umuhimu wa kisiasa au kihistoria mara nyingi huongeza msisimko wa umati na kuwapelekea kushawishika na kufuata msimamo ya kundi.

## Dalili za saikolojia ya kundi

Wataalamu wanasema kuna ishara kadhaa zinazoonyesha kwamba kundi linaanza kuendeshwa na saikolojia ya umati. Miongoni mwao ni hisia ya kuwa kundi halikosei kamwe, kupuuzwa kwa maoni tofauti, na watu kujinyamazia hata wanapohisi jambo fulani si sahihi.

Wakati mwingine kundi hujenga imani kwamba linafanya jambo la kimaadili hata kama linavunja sheria au kuumiza wengine. Hapo ndipo hatari huongezeka.

## Jinsi ya kupunguza athari zake

Kuelewa saikolojia ya kundi ni hatua ya kwanza ya kuizuia. Watafiti wanashauri kuwepo kwa mazingira yanayoruhusu watu kutoa maoni tofauti bila kuogopa. Elimu kuhusu upendeleo na propaganda pia husaidia watu kufikiria kwa utulivu hata wanapokuwa kwenye kundi.

Katika ngazi ya jamii, njia bora ni kushughulikia malalamiko halisi ya wananchi kabla hayajageuka hasira ya pamoja. Pale watu wanapopata njia salama za kueleza hisia zao, hakika uwezekano wa vurugu pia hupungua.

## Somo muhimu

Saikolojia ya kundi inaonyesha jambo muhimu kuhusu binadamu: mtu mmoja anaweza kuwa mtulivu, lakini watu wengi wakikusanyika wanaweza kuwa nguvu tofauti kabisa. Hii si hadithi ya watu wabaya pekee; mara nyingi ni matokeo ya mazingira, hisia, na shinikizo la kijamii.

Kwa hiyom swali si kama saikolojia ya kundi ipo. Ipo kila mahali—kwenye siasa, michezo, mitandao ya kijamii, na hata katika maisha ya kila siku. Swali muhimu zaidi ni kama tunaweza kuitambua mapema na kuizuia isigeuke nguvu ya uharibifu.



# Biashara halal ya mtandaoni: mwongozo wa kuanza bila mtaji mkubwa

**Katika miaka ya hivi karibuni, biashara za mtandaoni zimebadilisha namna watu wanavyopata kipato. Kwa Waislamu wengi, swali si tu jinsi ya kupata pesa, bali jinsi ya kupata kipato kilicho halali, safi na chenye baraka.**

**Habari njema ni kwamba kuanzisha biashara ya mtandaoni inayofuata misingi ya Kiislamu si jambo gumu kama wengi wanavyodhani. Kimsingi, kinachohitajika ni nia sahihi, mpango rahisi na uamuzi wa kufanya biashara kwa uadilifu.**

## Biashara halali ni ipi?

Katika mtazamo wa Kiislamu, biashara ya halali ni ile inayozalisha kipato kwa njia iliyo wazi, ya haki na isiyo na udanganyifu. Haitegemei riba, haiuzi bidhaa au huduma zinazodhuru watu, na haiahidi kitu ambacho haiwezi kukitoa.

Kwa lugha rahisi, ni biashara inayoheshimu wateja na kumheshimu Mwenyezi Mungu. Wateja wanajua wanachonunua, bei iko wazi, na muuzaji anasimama nyuma ya kile anachokiuza. Wataalamu wa uchumi wa Kiislamu mara nyingi husema kuwa biashara ya halali haiepuki tu yaliyo haramu, bali huchagua njia inayozalisha baraka katika maisha.

## Kwa nini biashara ya mtandaoni?

Tofauti na biashara za kawaida, biashara ya mtandaoni huondoa vikwazo vingi vinavyowazuia watu kuanza. Mara nyingi huhitaji mtaji mdogo, hakuna kodi ya pango la duka, na mtu anaweza kuanza akiwa nyumbani huku akiendelea na kazi nyingine.

Teknolojia pia imefungua milango ya soko la kimataifa. Mtu aliyeko Dar es Salaam anaweza kutoa huduma kwa mteja aliyeko Dubai, London au Kuala Lumpur. Hali hii imeifanya biashara ya mtandaoni kuwa fursa muhimu kwa vijana, wazazi wanaofanya kazi nyumbani, na hata wataalamu wanaotafuta kipato cha ziada.

## Njia tano maarufu za kupata kipato cha halali mtandaoni

Njia ya kwanza ni ajira za kujitegemea (freelancing). Hapa mtu huuza ujuzi wake moja kwa moja kwa wateja. Huduma zinazohitajika sana ni uandishi, uhariri, usanifu wa picha, programu za kompyuta, tafsiri na usaidizi wa kazi za ofisini kwa njia ya mtandao. Mfumo huu ni rahisi kuelewa: mnakubaliana kazi, mnafanya kazi, kisha unalipwa.

Njia ya pili ni kazi zinazohusiana na AI. Ingawa mashine zina uwezo mkubwa, bado zinahitaji binadamu kukagua kazi zake. Watu wengi sasa hulipwa kukagua maandishi yaliyotengenezwa na AI, kupanga data, au kutathmini ubora wa matokeo ya mifumo ya kidijitali. Mradi kazi hiyo haihusishi maudhui haramu, inaweza kuwa chanzo kizuri cha kipato.

Njia ya tatu ni biashara ya mtandaoni (e-commerce). Hii inaweza kuwa kuuza bidhaa halisi kama mavazi, vitabu au bidhaa za ubunifu. Pia inaweza kuwa bidhaa za kidijitali kama vile vitabu pepe, kozi au mifumo ya kazi. Kanuni muhimu hapa ni uwazi kuhusu bidhaa, bei na usafirishaji.

Njia ya nne ni kutengeneza maudhui. Blogu, video za elimu, au kurasa za maarifa zinaweza kuwa biashara ikiwa zinaaminika na zina msaada kwa jamii. Mapato yanaweza kutoka kwa matangazo, ushirikiano na biashara halali au uuzaji wa bidhaa zako mwenyewe.

Njia ya tano ni ufundishaji mtandaoni. Watu wanaweza kufundisha lugha, masomo ya shule, ujuzi wa kazi au hata masomo ya dini. Mfumo wake ni rahisi: maarifa yanabadilishwa kuwa huduma, na mteja analipa kwa kile anachojifunza.

## Kanuni ya "ngamia" katika biashara

Katika ulimwengu wa mitaji ya biashara, wawekezaji wengine hutumia mfano wa "ngamia" badala ya "nyati". Nyati huwakilisha kampuni zinazokua kwa kasi kubwa kwa kutumia fedha nyingi za mikopo au wawekezaji. Ngamia, kwa upande mwingine, hukua polepole lakini kwa uthabiti.

Biashara nyingi za halali hufuata mantiki ya ngamia. Zinajengwa juu ya kazi halisi, faida ya taratibu na nidhamu ya matumizi. Lengo si umaarufu wa haraka bali uwezo wa kudumu hata wakati soko linapobadilika.

## Usimamizi wa fedha baada ya kuanza kupata kipato

Kupata pesa kwa njia halali ni hatua ya kwanza. Hatua inayofuata ni kuzisimamia kwa maadili. Hii inamaanisha kuepuka riba, kuweka rekodi za mapato na matumizi, na kukuza biashara kwa kasi inayoweza kudhibitiwa.

Wataalamu wa fedha za Kiislamu pia wanashauri kutumia mifumo ya kifedha inayozingatia Sharia inapowezekana, pamoja na kutenga fedha kwa kodi au majukumu mengine mapema.